KWA JINA LA ALLAAH, MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

# Al-Hudaa [Uongofu]

# الهدى

Volume 11, Issue 3
15th RAJAB 1432
17th June, 2011

YALIYOMO

UHARAMU WA NYIMBO 1 - 4

## UHARAMU WA NYIMBO

Mtayarishi: Sheikh Sa'd ad-Deen ibn Muhammad al-Kibbi

### USHAHIDI WA UHARAMU WA MZIKI KUTOKA KATIKA QUR'AN NA SUNNAH

Amesema Allaah (سبحانه وتعالى): [**Na katika watu wako wanakhitari maneno ya upuzi ili wawapoteze watu na njia ya Allaah, pasipo wao kujua lolote, na wanaicheza shere hiyo njia ya Allaah basi hao watapata adhabu ifehedhishao (Luqman-6) ].**

Mwanachuoni wa Ummah Ibn 'Abbaas (رضي الله عنه) amesema: [Maana yake ni kuimba. Mujaahid (رضي الله عنه) amesema: [Hii yamaanisha kupiga ngoma (*tabl*) (Tafseer al-Tabari, 21/40)

Al-Hasan al-Basr (رضي الله عنه) amesema: Ayah hii iliteremshwa kuhusiana na kuimba na ala ya mziki [Tafseer ibn Katheer, 3/451].

**Al-Sa'di** (رضي الله عنه) amesema: [Hii yakusanya mambo yote ya maneno ya haramu, maneno ya upuzi na urongo, na kila sampuli ya upuzi wenye kuhamasisha kufr na ma'asiya; maneno ya wale wanaosema kauli za kupinga ukweli na kujadili kwa kuunga mkono urongo ili kuushinda ukweli; na kusengenya, na kuchafua majina, urongo, matusi na kulaani; kuimba na ala za mziki za shaytaan; na ala za mziki ambazo hazina faida yoyote ya kiroho wala faida ya ulimwengu. [Tafseer al-Sa'di, 6/150].

Ibn al-Qayyim (رضي الله عنه) amesema: [Tafsiri ya Maswahaba na Taabi'een, yakwamba 'maneno ya upuzi' yanahusiana na kuimba, inatosha. Hii imehadithiwa kwa isnaad zilizo swaheeh kutoka kwa Ibn 'Abbaas (رضي الله عنه) na Ibn Mas'ood (رضي الله عنه). Abu'l-Sahbaa' amesema: [Nilimuuliza Ibn Mas'ood (رضي الله عنه) kuhusu ayah hii [Luqman - 31:6], akasema: "Wallaahi, ambaye hapana mola mwengine asiyekuwa Yeye, maana yake ni kuimba- na alirudia hayo mara tatu.

Vile vile imepokewa kwa isnaad iliyo swaheeh kutoka kwa Ibn Umar (رضي الله عنه) kuwa hii yamaanisha kuimba. Hakuna utata baina ya tafsiri ya "maneno ya upuzi" kumaanisha kuimba na tafsiri yake kumaanisha visa vya wafursi na wafalme wao, na wafalme wa kirumi, na mengineyo, kama al-Nadri ibn al-Haarith aliyekuwa

*(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)*

## قافلة الرحمة للحج والعمرة Al-Rahma `Umrah & Hajj

**Agencies1432 Hijri / 2011 C.E**

**Assalaamu `Alaykum Warahmatullaahi Wabarakaatuh:**

Tunafuraha kuwajulisha yakwamba Insha Allaah Safari yetu ya mwaka huu 1432 Hijri/2011 ya kupeleka watu `Umrah katika mwezi wa Ramadhaan, kumi la mwisho. Na vilevile katika `Ibaadah ya Hijjah.

Mipangilio ya Safari ya `Umrah (Mwezi wa Ramadhaan) ni kama ifuatayo:

• Kuondoka ni tarehe 17 ya mwezi wa Ramadhaan*Kurudi ni baada ya `Eid Insha Allaah

• Safari itaanzia Nairobi – Jeddah

• Gharama ya Safari (ikiwemo Hoteli na Usafiri) ni $1500 U.S

• Siku tatu tutakuwa Madinah na Siku kumi za mwisho tutakuwa Makkah mpaka `Eid.

• Safari ya Kurudi Jeddah – Nairobi. Itakuwa baada ya `Eid

Twapenda kuwahimiza wale wale wenye niya ya kwenda na sisi waharakishe kuleta Passport zao na picha Nne kwa ajili ya kufanya maandalizi. Sababu ni kwamba Viza zitafungwa kabla ya mweizi wa Ramadhaan kuanza.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa njia zifuatazo:

• Tutumie e-mail katika info@qssea.net au

• Simu nambari +254 723471820 (Abu Bilaal Athman Na'man)

• Simu nambari +254 721473181 (Abu Farida Muhammad Basawad)

*(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)*

akiwaeleza watu wa Makkah ili awashughulishe wasipate kuisikiliza Qur'an, yote hayo mawili ni maneno ya upuzi. Ndipo Ibn Abbaas akasema: "maneno ya upuzi" ni urongo na kuimba. Baadhi ya Maswahaba wamesema hili na wengine wakasema jengine, na wengine wakasema yote mawili. Kuimba ni uovu zaidi kuliko visa vya wafalme, kwa sababu yapelekea kwenye uzinifu na kuukuza unafiki ukuwe (ndani ya nyoyo); ni mtego wa Shaytaan, na huziba fahamu zetu. Namna inavyowazuia watu wasiwe karibu na Qur'an ni vibaya zaidi kuliko yalivyo maneno mengine ya urongo yanavyowazuia, kwa sababu watu kwa kawaida ni wenye asili ya kuelekea kwenye hizo nyimbo na huwa na hamu kubwa ya kupendelea kutaka kusikiliza. Aya inashutumu kuibadilisha Qur'an kwa maneno ya upuzi ili kupoteza watu na njia ya Allaah (sw) bila ya 'ilmu na kuichukuwa kama mzaha, kwa sababu Ayah ya Qur'an ikisomwa kwa mtu kama huyo, hugeuza mgongo wake kama ambaye hakusikia, kama kwamba ana uziwi katika masikio yake. Akisikia chochote kutoka kwenye Qur'an hulifanyia hilo mzaha. Yote haya yatokea pekee kwa watu ambao ni makafiri wakaidi mno na kama baadhi yake hutokea kwa waimbaji na wanaowasikiliza, wote hao huwa na ushirika katika lawama hii. *(Ighaathat al-Lahfaan, 1/258-259)*

Amesema Allaah (سبحانه وتعالى):[**Na wavute uwawezao miongoni mwao kwa sauti yako**] (yaani nyimbo, mziki, na kila mwito wa kumu'asi Allaah) ..." [al-Israa' 17:64]

Imehadithiwa kuwa Mujaahid (رحمه الله) amesema: "Na wavute kwa sauti yako (sauti ya Iblees) ni kuimba na urongo. Ibn al-Qayyim (رحمه الله) amesema idaafah (possessive or genitive construction yaani sauti yako) yatosheleza kuifanya maana iwe haswa, kama neno "jeshi lako la waliopanda" na jeshi lako wanaotembea" (baadaye katika aya hio hio). Kila anayezugum,za kwa njia yoyote ya maasi kwa Allaah. Kila anaye puliza zumari au ala nyingine za kupuliza au achezae ngoma zozote za haramu, hii ni sauti ya Shaytaan. Yoyote anayetembea kuelekea kwenye kumuasi Allaah ni katika mkao wa Shaytaan jeshi la miguu (infantry). Yoyote anayepanda kufanya dhambi ni katika mkao wa Shaytaan jeshi lake la waliopanda (cavalry) haya ndio maoni ya Salaf, kama alivyo haditjhia Ibn Abi Haatim kutoka kwa Ibn Abbaas "jeshi lake la miguu ni kila anaye tembea kumuasi Allaah". (*Ighaathat al-Lahfaan*).

Allaah asema: "**Je mnaistaajabu Hadithi hii?*Na mnacheka wala hamlii*Na mmeghafilika tu-** (an-Najm 53:59-61)

Ikrima (رحمه الله) amesema: "Imehadithiwa kutoka kwa Ibn 'Abbaas kuwa al-Sumood (neno linaloashiriya kitendo kutokamana na 'Saamidoon') limefasiriwa kuwa ni "kupoteza umri wako wa thamani katika kupitisha wakati na kujifurahisha (kuimba)' yamaanisha kuimba katika lahja ya Himyar; hwenda ikasemwa "Ismidi lanaa" (tuimbie - kutoka kwenye asili hiyohiyo kama saamidoon/sumood ikimaanisha "ghaniy" (imba) na akasema (رحمه الله): "Wakati makafiri walipoisikia Qur'an, walikuwa wakiimba, kisha ayah hii ikateremshwa."

Ibn Katheer (رحمه الله) akasema: "Allaah amesema: 'Kupoteza umri wako wathamani kwa kupitisha wakati na kujipumbaza (kuimba au kusikiliza mziki)".

Sufyaan ath-Thawree amesema akihadithia kutoka kwa babake kutoka kwa Ibn 'Abbaas (رضي الله عنه): "Maana yake ni kuimba. Hii ni lahja ya ki-Yemeni: Ismad lana yamaanisha ghan lana (tuimbie), haya pia yalikuwa ni maoni ya Ikrimah (Tafseer ibn Katheer).

Imehadithiwa kutoka kwa Abu Umaamah (رضي الله عنه) kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Musiwauze vijakazi wenye kuimba, musiwanunue wala musiwafunze, hakuna lolote zuri katika biashara hii na thamani yao ni haramu. Kuhusu hayo Ayah hii ikateremshwa (Luqman-31:6) (hadeeth hassan)

Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Hakika miongoni wa Ummah wangu kuna watakaohalalisha Zinaa, hariri, pombe na ala za mziki..." (imepokewa na al-Bukhari *ta'leeqan,* no. 5590; ikapokewa kwa njia mawsool na at-Twabaraani na al-Bayhaqee. Angalia al-Silsilah al-Swaheehah cha al-Albaani, 91).

Ibn al-Qayyim (رحمه الله) amesema: Hii ni hadeeth swaheeh iliyopokewa na al-Bukhaari katika swaheeh yake, alipoinukuu kama ushahidi na akasema yakwamba ni *mu'allaq* na *majzoom*. Akasema katika mada ya yaliohadithiwa kuhusu wanaoruhusu pombe na kuliita kwa jina jengine.

Hadeeth hii yaonyesha kwa njia mbili kuwa ala za mziki na starehe ya kusikiliza mziki ni haraam. La kwanza ni uhakika wakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliposema: "[wao] wahalalisha", jambo lenye kuashiriya wazi-wazi yakwamba vitu vilivyotajwa miongoni mwavyo vikiwemo ala za mziki ni haraam kulingana na sharee'ah, lakini hao watu watahalalisha. La pili ni kuwa ala za mziki zimetajwa pamoja na vitu vinavyojulikana kuwa haraam kama vile zinaa na pombe: ikiwa ala za mziki zilikuwa si haraam, basi ni kwanini vitajwe pamoja na vilivo haraam? {imetolewa kutoka kwa al-Silsilah al-Swaheehah cha al-Albani, 1/140-141}

Ibn Taymiyah (رحمه الله) amesema: "Hadeeth hii yaonyesha kuwa ma'aazif ni haraam na ma'aazif yamaanisha ala za mziki kulingana na wanavyuoni wa lugha ya Kiarabu. Neno hili lakusanya ala zote mfano wake." (al-Majmoo;11/535)

Ibn al-Qayyim (رحمه الله) amesema:

*(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)*

*(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)*

“Kulingana na somo hilo hilo maneno yalio sawa yamehadithiwa kutoka kwa Sahl ibn Sa’d al-Saa’idi, Imraan ibn Husayn, Abdullaah ibn ‘Amr, Abdullaah Ibn ‘Abbaas, Abu Hurayrah, Abu Umaamah al-Baahili, Aa’shah Umm al-mu’mineen, Ali ibn Abee Twaalib, Anas ibn Maalik, Abdur-Rahmaan Ibn Saabit na al-Ghaazi Ibn Rabee’ah (رضي الله عنهم). Kisha akataja katika *Ighaathat al-Lahfaan* na yaonyesha kuwa ala za mziki ni haraam.

Imehadithiwa kuwa **Naafi’** (رحمه الله) amesema: “Ibn Umar iliisikia firimbi ya mti ikipulizwa (zumari) akatia vidole mashikioni mwake na akabadilisha njia. Akaniambia mimi, “Ewe Naafi’ wasikia chochote?” Nikasema, “Laa”, basi akatoa vidole vyake kutoka mashikioni mwake na akasema: “Nilikuwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) na akasikia kitu kama hicho na akafanya kama nilivyofanya.” (swaheeh Abi Dawood).

Mtu mmoja aliye duni, amesema hadeeth hii haionyeshi uharamu wa ala za mziki, kwa sababu ikiwa ni hivyo Mtume (صلى الله عليه وسلم) angemuamrisha Ibn Umar (رضي الله عنه) kutia vidole vyake mashikioni pia na Ibn Umar angemuamuru Naafi’ nae kufanya hivyo. Jibu kwa hili ni kwamba alikuwa hasikilizi, lakini alikuwa akisikia. Kuna tafauti baina ya kusikiliza na kusikia.

Ibn Taymiyah (رحمه الله) amesema: “Kuhusu mziki ambao mtu hana nia ya kusikiliza hakuna makatazo wala lawama kulingana na maafikiano ya wanazuoni. Kwahiyo lawama au kusifiwa imefungamana na kusikiliza sio kusikia. Yule anayesikiliza Qu’an atalipwa ujra kwa kuisikiliza, haliyakuwa mwenye kuisikia bila ya kutaka au kukusudia kuisikiliza hatalipwa ujra, kwa sababu vitendo hulipwa kwa nia. Na hivyo ndivyo ilivyo pia kwa ala za mziki ambazo ni haraam. Ikiwa mtu atazisikia bila ya kukusudia basi haina neno (al-majmoo; 10/78).

Ibn Qudaamah al-Maqdisi (رحمه الله) amesema: “Msikilizaji ni yule anayekusudia kusikiliza, jambo ambalo halikuwa kumuhusu Ibn ‘Umar (رضي الله عنه); kilichofanyika kuhusu kisa chake ni kusikia. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alitaka kujua sauti kama imekoma kwa sababu aligeuza njia hiyo na akaziba mashikio yake. Kwahivyo hakutaka kurudi njia hiyo au kutoa vidole vyake mpaka sauti ipotee, kwa hivyo alimruhusu Ibn ‘Umar kusikia, ilikuwa ni dharura. (*al-Mughni,* 10/173)

Ingawa kusikia inayozingatiwa na Maimamu wawili ni makrooh iliruhusiwa kwa dharura kama tutakavyo-ona katika maneno ya Imaam Maalik na Allaah Ndiye Mjuzi zaidi.

## MAONI YA WANAVYUONI (MAIMAMU) WA KIISLAMU

Al-Qaasim (رحمه الله) amesema: “Kuimba ni katika sehemu ya urongo.” Al-Hasan (رحمه الله) amesema: “Ikiwa kuna mziki kwenye ualishi wa Waleemah, usikubali ualishi huo (*al-Jaami* cha *al-Qayrawaani*, Uk. 262-263).

Ibn Taymiyah (رحمه الله) amesema: “Maoni ya Maimaamu wote wanne ni kwamba vyombo (ala) sampuli zote za mziki ni haraam. Imehadithiwa kutoka kwenye swaheeh al-Bukhaari na kwengineko yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema kuwa miongoni mwa ummah wake, watu watakaoruhusu zinaa, hariri, pombe, na ala za mziki, na akasema yakwamba watabadilishwa wawe Manyani na Nguruwe ... Hakuna katika wafuasi wa maimaam aliyeleta ubishi katika jambo hili kuhusu mziki. (al-majmoo; 11/576).

Al-Albaani (رحمه الله) amesema: “Madhehebu yote manne yakubaliana kuwa ala zote za mziki ni haraam. (as-Swaheeha, 1/145).

Ibn al-Qayyim (رحمه الله) amesema: “Madhehebu ya Abu Haneefah (رحمه الله) ndiwo wagumu zaidi kuhusu hili na maoni yake ni miongoni mwa maoni yaliyo makali zaidi. Wanafunzi wake wamesema wazi kuwa ni haraam kusikiliza ala zote za mziki kama zumari na ngoma, hata kupiga kijiti. Wamesema kuwa ni dhambi lenye kudokeza yakwamba mtu ni fasiq ambaye ushahidi wake haufai kukubaliwa. Wakenda zaidi ya hapa wakasema kuwa kusikiliza mziki ni fisq na kustarehe nao (mziki) ni ukafiri. Haya ni maneno yao. Wanahadithia kuunga mkono hadithi hizo ambazo haikuwezekana kuzinasibiisha na Mtume (صلى الله عليه وسلم). Wakasema: “Na ajaribu mtu asisikie akiwa ni mpita njia au ataisikia katika mtaa wake.” Abu Yoosuf amesema: “Kuhusu nyumba ambayo waweza kusikia ala za mziki ndani yake, ingia ndani bila ya idhni yao kwa sababu kukataza vitendo vibaya ni waajib, na lau kama ingelikuwa hairuhusiwi kuingia bila idhni yao, watu hawangeliweza kutimiza wajibu wao wa kuamrisha mema na kukataza maovu. (*Ighaathat al-Lahfaan,* 1/425)

Imaam Maalik (رحمه الله) aliulizwa kuhusu kupiga ngoma au kupuliza zumari, ikiwa mtu ataisikia sauti na akastarehe (akaburudika) akiwa atembea au amekaa. Akasema: “Na asimame ikiwa atajiona yakwamba inampumbaza, ila akiwa amekaa kwa dharura au hawezi kusimama. Lau akiwa barabarani anafaa arudi au ataendelee kwenda mbele.” (*al-Jami’* cha *al-Qayrawaani*, 262). Yeye (رحمه الله) akasema: “Watu wanaofanya hivyo (kusikiliza mziki) kwa maoni yetu ni watu *mafaasiq* peke yake. (*Tafseer al-Qurtubi,* 14/55)

Ibn Abdul-Baar (رحمه الله) amesema: “Miongoni mwa mapato ya haraam kwa maafikiano ya wanazuoni ni ribaa, ujira wa kahaba, chochote kilicho haramishwa, hongo, malipo ya mwenye kuomboleza (kulia matangani kwa malipo) na kuimba, malipo kwa wapiga ramli na wale wanaodai kujua yasioonekana (*ghaib*) na

*(Endelea Kwenye Ukurasa wa 4)*

*(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)*

watu wa falaki (*astrologers*) malipo ya wapigaji zumari na (mziki kwa jumla) na kamari." (*al-Kaafi*).

Ibn al-Qayyim (رحمه الله) amesema akieleza maoni ya Imaam ash-Shaafa'i (رحمه الله): "Wanafunzi wake wanaojua (rai zake) madhehebu yake wamesema kuwa ni haraam na wakawashutumu wale wanaosema yakwamba alililiruhusu hilo. (*Ighaathat al-Lahfaan*, 1/425)

Mwandishi wa *Kifaayat al-Akhbaar*, ambaye alikuwa ni mmoja wa ash-Shaafa'i alihesabu ala za kimziki kama zumari na vyengine kuwa ni vitu viovu, na aliyehudhuriya (kuwepo zinapochezeshwa) na azilaumu na kuzikashifu. (Hawezi kupewa udhuru kwa kuwa kuna wanavyuoni waovu, kwa sababu wafisidisha Sharee'ah au faqeer waovu - kumaanisha ma-Sufi, kwa sababu wao wajiita fuqaraa' au ma-faqeer - kwa sababu wao ni wajinga na humfuata yoyote afanyaye fujo, na kupiga kelele; hawakuongoka kwa nuru ya 'ilmu; bali wamepeperushwa na kila upepo ujao. (*kifaayat al-Akhbaar*, 2/128).

Ibn al-Qayyim (رحمه الله) amesema: "Amma kuhusu maoni ya Imaam Ahmad (رحمه الله): mwanae 'Abdullaah (رحمه الله) amesema: 'Nilimuuliza babangu kuhusu kuimba, akanijibu, kuimba hukuuza unafiki moyoni ; mimi silipendi jambo hilo, kisha akataja maneno ya Maalik: watu waovu (ma-faasiq) miongoni mwetu wafanya hayo. ( *Ighaathat al-Lahfaan*)

Ibn Qudaamah (رحمه الله), mtafiti wa madhehebu ya Hanbali amesema: "Ala za mziki ni za sampuli tatu ambazo ni haraam, nazo ni nyuzi na sampuli zote za zumari (tarumbeta, saksafoni na mfano wake ) na rabaab ( gita,fidla na mifano yake). Yoyote mwenye kuzisikiliza, basi ushahidi wake usikubaliwe." (*al-Mughni,* 10/173). Na akasema (رحمه الله): "Na ikiwa mtu ataalikwa katika hafla ambapo patakuwa na kitu chenye kuchukukiza kama pombe na ala za mziki, na akawa aweza kuyapinga na kuyakataza, basi na ahudhurie na azungumze dhidi yao, kwa sababu atakuwa ameunganisha mambo mawili katika wajibu. Akiwa hawezi kufanya hivyo, basi asihudhurie. (*al-Kaafi,* 3/118)

Al-Twabaree (رحمه الله) amesema: "Wanazuoni wa maeneo yote wameafikiana kuwa kuimba ni makrooh na yafaa ikatazwe. Hata kama Ibraahim Ibn Sa'd na 'Ubaydullaah al-Anbaree wamekhitilafiana na kundi kubwa la wanavyuoni, (inafaa kutanabahishwa yakwamba) Mtume ( صلى الله عليه وسلم) amesema: "Shikamana na Jama'ah". Na yoyote atakaekufa haliyakuwa ametengana na Jama'ah na Jama'ah, atakufa kama jaahil. (Tafseer al-Qurtubi, 14/56). Katika vizazi vya zamani "**MAKROOH**" ilikuwa ikitumiwa kumaanisha **HARAAM** kisha ikachukua maana ya "kuchukia". Lakini hii inataka ifahamike kumaanisha kuwa imekatazwa. Kwa sababu yeye (at-Twabaree) amesema: "yafaa izuiliwe" na hakuna kifaacho kuzuiwa ila kilicho haraam. na kwa sababu katika hadeeth mbili zilizotajwa awali, mziki umekashifiwa kwa maneno makali mno. Al-Qurtubi ( رحمه الله) ndiye aliyepokea hadeeth hii, kisha akasema: "Abu'l-Faraj na al-Qaffaal (رحمهم الله) miongoni mwa ma-swaahib zetu wamesema: "Ushahidi wa muimbaji na mchezaji mziki haufai kukubaliwa. Mimi nasema: Ikiwa itathibitishwa kuwa si halali basi kupokea malipo kutokamana na shughuli hizo vilevile itakuwa ni haramu.

### Amesema Shaykh al-Fawzaan (حفظه الله):

"Waliyoyasema Ibraheem Ibn Sa'd na 'Ubaydullaah al-Anbaree (رحمهم الله) kuhusu kuimba si kama kuimba kwa siku hizi, kwani wao hawangeruhusu sampuli hii ya uimbaji iliyo na uovu na uchafu wa kupindikia. (*al-I'laam*)

Ibn Taymiyah (رحمه الله) amesema: "Hairuhusiwi kuunda ala za mziki (al-*Majmoo'* 22/140) na akasema: "Kulingana na wengi katika ma-Fuqahaa, yaruhusiwa kuvunja vifaa vya mziki kama tanboor (chombo fulani cha mziki kilichofungwa nyuzi [mandolin]). Haya ni maoni ya Maalik (رحمه الله) na ndiyo mashuhuri baina ya rai mbili zilizopokewa na Ahmad ( رحمه الله)." (*al-Majmoo'* 28/113). Na akasema: "Ibn al-Mundhir alitaja kuwa wanavyuoni wameafikiana kuwa hairuhusiwi kuwalipa watu kwa kuimba na kulia ..., maafikiano ya wanavyuoni wote ambao maoni yao tumejifunza ni kwamba kuimba na kuomboleza (wanao omboleza kama kazi) hairuhusiwi." Al-Shu'bi, al-Nakha'i na Maalik wamehukumu yakwamba jambo hilo ni Makrooh (yaani haraam). Abu Thawr, al-Nu'maan, abu Haneefah (رحمهم الله), na Ya'qoob na Muhammad wanafunzi wawili wa Abu Haneefah wamesema: 'Hairuhusiwi kulipa chochote kwa kuimba wala kuomboleza. Hii ndio rai yetu.' Na wakasema: 'Ala za mziki ni ulevi wa roho, na inachofanya rohoni ni uovu zaidi kuliko vyenye kulewesha vinavyofanya. (*Majmoo al-Fataawa* 10/417).

**ENDELEA KATIKA MAKALA YAJAYO**

JIPATIE NAKALA YA KITABU CHA SWALA:

NAMBARI ZA SIMU NI:

0721473181 AU 0727341779

MOMBASA